



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MVDC/F.30/16 VOL. I/29

Tarehe: 08/04/2025

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
S. L. P 938,
DAR ES SALAAM.

**YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED
(VCSL) INAYOTEKELEZA MRADI KATIKA WILAYA YA MVOMERO.**

Rejca kichwa cha habari hapo juu chahusika.

1. Naitambulisha kwako Kampuni tajwa hapo juu, inayotekeleza Mradi wa Biashara ya Kaboni kupitia mfumo unaojulikana kama “Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji miti hovy na Uharibifu wa Misitu” (MKUHUMI) kwa malengo ya kuwezesha vijiji mbalimbali hapa Tanzania vikiwemo vya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.
2. Mpango huu unasaidia kuimarisha uhifadhi wa Misitu ya Asili inayomilikiwa na Vijiji, kwa mujibu wa Vifungu namba 4 (c) (i), 32 (1) (a) na (b) na 35 (6) (b) vya Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002 ya Tanzania.
3. VCSL inashirikiana na Vijiji na Halmashauri ya Mvomero kutekeleza MKUHUMI kwa lengo la kuzalisha na kuuza kredit za Kaboni, ambapo vijiji vitapata fedha zitakazosaidia maendeleo ya jamii hususani kuboresha kilimo, elimu ya sekondari na ufundi, afya, maji na upatikanaji wa hati miliki za ardhi.
4. Mradi wa VCSL unajulikana kama Village Climate Solutions Project (VCSP) na umesajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mfumo wa Kimataifa wa Viwango vya Kaboni (Verified Carbon Standards - VCS) na Viwango vya Ubora (Climate, Community and Biodiversity – CCB standards) kupitia akaunti namba 1325.
5. Katika Wilaya yetu, Mradi huu unatekelezwa katika vijiji vya Maharaka, Sewekipera, Miscengele, Kihondo na Msongozi (Rejca Ramani iliyoambatishwa).

Halmashauri ya Wilaya Mvomero, S.L.P. 663, Morogoro, Simu: +255232934348, Nukushi: +2552334348,
Barua pepe: ded@mvomerodc.go.tz, tovuti: www.mvomerodc.go.tz

6. Ninaomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kushirikiana na Kampuni ya VCSL katika masuala yote yanayohusiana na uwekezaji na utekelezaji wa mradi huu wa Kaboni ili kuhakikisha mafanikio yake na manufaa kwa jamii yanafikiwa.
7. Natarajia ushirikiano wako.

Ahsante.



Loema P. Isaay

**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO**

Nakala: Katibu Tawala wa Wilaya ya Mvomero
S.L.P 59 MVOMERO,
MOROGORO.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO
S.L.P 663, MOROGORO

Halmashauri ya Wilaya Mvomero, S.L.P. 663, Morogoro, Simu: +255232934348, Nukushi: +2552334348,
Barua pepe: ded@mvomerodc.go.tz, tovuti: www.mvomerodc.go.tz

